# KIJARIDA CHA BANGO




TOLEO
JIPYA

JULAI - SEPTEMBA
2023

# MKUTANO MKUBWA WA VYOMBO VYA HABARI KUFANYIKA ZANZIBAR




Zaidi ya watu 200 kutoka nchi mbalimbali ndani na nje ya Bara la Afrika watashiriki katika mkutano mkuu wa mwaka wa Umoja wa Mashirika ya Utangazaji ya Umma Kusini mwa Afrika (SABA) utakaofanyika Zanzibar tarehe 10 – 12 Oktoba, 2023.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) Dkt. Ayub Rioba Chacha amesema lengo la mkutano huu ni kujadili namna bora ya kukuza Teknolojia ya Habari na Utangazaji katika vyombo vya habari vya Umma na kuwezesha vyombo hivi kuendelea kuwepo na kuzidi kupata hadhira.

Dkt. Rioba amesema hayo katika mkutano na Waandishi wa Habari uliofanyika katika ofisi za TBC Mikocheni mjini Dar es Salaam.

Amesema, mkutano huu utawakutanisha Wakuu wa Vyombo vya Habari vya Umma kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na wadau wa TEHAMA kutoka ndani na nje ya bara la Afrika.

Mgeni rasmi katika mkutano huu wa SABA anatarajiwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

# TBC KUWEKA KUMBUKUMBU YA MAENDELEO - SABASABA




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nape Nnauye ameitaka TBC kutengeneza makala maalumu ambayo itaeleza hatua kwa hatua maonesho ya Kimataifa ya Biashara – SABASABA yalivyoboreshwa toka yaanze mpaka sasa.

Waziri Nape ameipongeza TBC kwa kuwa mstari wa mbele kutangaza maonesho hayo kupitia vyombo vyake vya televisheni, radio na mitandao ya kijamii na kuwahimiza Maafisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutumia maonesho hayo kama fursa ya kukuza uchumi wa Kidijiti

Pia ameielekeza Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade) kuboresha maonesho ya Sabasaba yajayo kwa kuongeza matumizi ya teknolojia.




"Uchumi wa Kidijiti haukwepeki, lazima sheria zetu, sera, kanuni zifanane na mikakati ya sera na kanuni za dunia kidijitali" Amesema Waziri Nape.

Ameongeza kwamba kuanzia maonesho ya mwaka 2024 viwanja vya Sabasaba viwekwe anuani za makazi ili mtu akiingia aelekezwe kwa vibao na kusisitiza matumizi ya vifaa vya kidijiti kuonesha ramani za maeneo mbalimbali katika maonesho hayo.

Waziri Nape ameyasema hayo akizungumza na wadau mbalimbali wa Habari na Teknolojia zikiwemo Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hiyo katika maadhimisho ya siku ya TEHAMA katika maonesho ya SABASABA.

# ZIARA YA WAZIRI KAIRUKI TBC



Utafiti na ubunifu wa uendeshaji ni muhimu sana katika kuhakikisha chaneli ya Tanzania Safari inafika kote duniani na katika ubora unaotakiwa.

Waziri wa Maliasili na Utalii Mh. Angela Kairuki amesema hayo tarehe 25 Septemba, 2023 alipotembelea ofisi za Shirika la Utangazaji Tanzania, TBC zilizopo Mikocheni jijini Dar Es Salaam.

Amesema TBC ifanye utafiti namna mataifa yenye chaneli za Utalii kama ilivyo TBC yamekua yanaendesha chaneli hizo ili kuiendesha Channel hiyo kisasa zaidi.

Mheshimiwa Kairuki amepongeza juhudi zinazofanywa na uongozi wa TBC kupitia chaneli hiyo katika kukuza na kuendeleza utalii nchini.



Akitoa taarifa fupi ya chaneli ya Tanzania Safari, Kaimu Mkurugenzi wa chaneli hiyo , Louisa Mtopwa amesema kwa sasa chaneli hiyo inatoa tafisiri ya matangazo yake kwa maandishi (subtitles) kwa lugha tano ambazo ni Kifaransa, Kichina, Kiarabu, Kiingereza na Kireno lengo likiwa ni kuongeza wigo wa watazamaji kutoka pande mbalimbali za dunia.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBC, Aisha Dachi amemshukuru Waziri Kairuki kwa kuitembelea na kuahidi kuyafanyia kazi maelekezo yote ambayo ameyatoa.

# TBC NA UNCDF KUELEMISHA MATUMIZI YA NISHATI MBADALA



Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo (UNCDF) kupitia mradi wa Cookfund, zinalenga kushirikiana na TBC kuelemisha jamii kuhusu matumizi ya nishati mbadala ili kuendana na mabadiliko ya tabia nchi ikiwemo utanzaji wa mazingira na kuondokana na madhara yatokanayo na nishati isiyo safi.

Mazungumzo kuhusiana na ushirikiano huo yamefanyika katika ofisi za TBC Mikocheni, Dar es salaam kati ya viongozi wa UNCDF wakiongozwa na Mtendaji Mkuu wake kwa hapa Tanzania, bwana Peter Malika na Mkurugenzi Mkuu wa TBC, Dkt. Ayub Rioba Chacha.




Mkuu wa UNCDF Tanzania Peter Malika amesema kupitia mradi wa nishati mbadala wanalenga kuiunga mkono Serikali katika jitihada za kuendeana na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na mpango wa Serikali wa kuelekea matumizi ya nishati mbadala kwa Taasisi zenye watu chini ya 100 kufikia mwaka 2024 na kwa Taasisi zenye watu chini ya 200 mwaka 2025 .

Dkt. Rioba amesema TBC imekuwa mstari wa mbele kusimamia, kutunza na kuelemisha jamii kuhusu utunzaji wa mazingira kupitia vipindi mbalimbali vinavyorushwa hapo.

# KOREA YATOA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA KWA WATENDAJI WA TBC




Shirika la Utangazaji Korea (KBS) na mamlaka ya udhibiti wa vyombo vya habari nchini Korea (RAPA) wametuma ujumbe wa wakufunzi kumi (10) kutoa mafunzo kwa watumishi wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kutoka vitengo vya uzalishaji vipindi, kamera na wahandisi kuhusiana na matumizi ya teknolojia katika uzalishaji wa vipindi bora.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Aisha Dachi amesema haya ni matokeo ya mkataba wa makubaliano wa kutoa mafunzo mbalimbali ya teknolojia katika uzalishaji wa vipindi ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani.

Mkataba huo kati ya TBC, KBS na RAPA ni wa mwaka mmoja.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Ufundi Mhandisi Upendo Mbelle amewashukuru RAPA kwa kutoa msaada wa ujenzi wa studio za kisasa za TBC2.

Mafunzo hayo yamefanyika kwa muda wa siku 14 kwa kuhusisha masomo ya darasani na vitendo.

# TBC YAONGOZA TUZO ZA UMAHIRI




Watumishi sita wa Shirika la Utangazaji Tanzania TBC wameibuka kidedea kwa kupata tuzo mbalimbali za umahiri katika habari na utangazaji. Tuzo hizo zimetolewa kwa nyakati tofauti katika nchi za Tanzania, Nigeria na Afrika Kusini.

Djaro Arungu alijinyakulia tuzo mbili ambazo ni tuzo ya Mtangazaji bora wa Kiume wa Radio kwenye tuzo za Shining Star 2023 na Tuzo ya Uandishi wa Habari za Afya upande wa Radio za EJAT 2022.

# TBC YAOGOZA TUZO ZA UMAHIRI




Gloria Michael amekuwa mshindi wa tuzo ya watu 100 wenye umri chini ya miaka 40 wenye mchango katika sekta ya Utalii, Khalid Gangana amejishindia tuzo ya mtangazaji bora wa kiume kipengele cha Televisheni, tuzo zilizotolewa Septemba, 2023 Afrika ya Kusini.

Wengine ni James Lerombo aliepata ushindi na kujinyakulia tuzo kwenye kipengele cha Habari za Utawala bora na uwajibikaji kwa upande wa luninga.

Mtangazaji Anna Peter amekua mshindi wa tuzo za EJAT 2022 katika kipengele cha habari za kilimo na biashara ya kilimo kwa upande wa luninga.

# TBC YAONGOZA TUZO ZA UMAHIRI




Aidha, mwandishi Peter Lugendo amepata ushindi wa tuzo ya Mwandishi wa habari za Afya ya uzazi kwa upande wa redio katika tuzo za EJAT 2022 zilizotolewa Julai, 2023 jijini Dar Es Salaam.

Mkurugenzi Mkuu Dr, Ayub Rioba Chacha anawapongeza wote waliopata tuzo hizo na kuwataka kuongeza bidii ili waweze kupata mafanikio zaidi kwa kuwa umahiri wao ndio uliopelekea ushindi huo ambao umelipatia heshima Shirika.